**Hotuba ya Salim Ahmed Salim Katika Kongamano la Kumbukumbu ya Miaka Kumi ya Kifo cha Mwalimu Nyerere lililoandaliwa na Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Jumatatu Tarehe 30 Novemba 2009, Ukumbi wa Karimjee, Dar Es Salaam, Tanzania.**

## SALAMU

Waheshimiwa wageni waalikwa.

Mabibi na mabwana.

## UTANGULIZI

Kwa niaba ya bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere na kwa niaba yangu binafsi, nawashukuru sana kuja kujumuika nasi tena leo katika muendelezo wa kongamano letu hili la Kumbukumbu ya Miaka Kumi tangia Baba wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kufariki dunia, kongamano ambalo limeaanza tangia jana.

Ninaamini kuwa wote kwa pamoja tumefika hapa kwa moyo mkunjufu kabisa ili kujumuika pamoja katika kukumbuka na kuenzi Maisha, Falsafa, Misingi na Dira ya Mwalimu Nyerere kwa Taifa letu, Bara letu na Dunia yetu kwa ujumla.

Kama alivyosema jana ndugu yangu Joseph Butiku, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere. Sisi wajumbe wa Bodi ya Wadhamini, tukitilia maanani hali ya kisiasa katika nchi yetu na dunia kwa ujumla, inayoambatana na hofu na mashaka kuhusu mustakabali wa Taifa letu. Tumeonelea ni vyema kuwakutanisha wadau mbalimbali nchini, kama hatua ya mwanzo ya kuanzisha Mjadala wa Kitaifa kuhusu Misingi ya Utaifa wetu na pia mustakabali mzima wa Taifa letu.

Kama ambavyo mmeona ama mmesikia tangia jana tulipoanza kongamano letu. Kwa hakika kuna mengi kutoka kwa Mwalimu Nyerere, ambayo Taasisi na Watanzania wote kwa ujumla, tunaweza kuyatumia ipasavyo katika kutekeleza jukumu letu la kupambana na changamoto tunazokumbana nazo na kuendeleza jitihada zetu za kujenga Taifa lenye kujali UTU na Maendeleo ya kila mmoja wetu, kama ambavyo waasisi wa Taifa letu walidhamiria.

Ni wazi kuwa kuna mengi ambayo tunaweza kujifunza kutoka kwa Mwalimu Nyerere ambayo yanatoa majibu thabiti yatakayoweza kutupa mwelekeo bora katika mapambano yanayoendelea dhidi ya maadui wakuu wa taifa letu, kama umasikini, ujinga, maradhi, ufisadi, siasa chafu, ubaguzi, ubinafsi na mengineyo.

**TANZANIA BAADA YA MWALIMU**

Ndugu wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana

Ni wazi kuwa baada ya miaka kumi ya kuondokewa na Baba wa Taifa letu, kama taifa kuna mambo mengi yametokea na yanayoendelea kutokea, ambayo yanatutaka sisi kama wadau wa taifa hili kuwa na uthubutu wa kuanzisha mchakato wa kujitazama, kujichunguza na kukubaliana jinsi gani tunaweza kujinasua katika majanga kadhaa yanayotunyemelea.

Wakati ambapo katika miaka ya hivi karibuni tumeweza kupata mafanikio kadhaa kama vile kupanuka kwa nafasi ya utoaji mawazo na maoni miongoni mwa jamii, kuongezeka kwa ushirikishwaji wa wananchi katika mfumo wa maamuzi nchini, kukua kwa nguvu za kiuchumi, kujengeka na kuboreka kwa mifumo na asasi za kiutawala, kukua kwa matumizi ya teknolojia hasa ile ya habari na mawasiliano katika taifa letu ambako kumeendana pamoja na kuongezeka kwa uhuru wa kutoa na kupata habari, na mengineyo

Vilevile tumekuwa tukikumbana na changamoto kadhaa kama vile kuporomoka kwa Maadili na Misingi ya Utaifa, Kuongezeka kwa umasikini na tofauti ya kipato kati ya wenye nacho na wasio nacho, Kuibuka kwa migawanyiko katika misingi ya makundi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, Kuibuka na kushamiri kwa utamaduni wa siasa chafu, kushuka kwa kiwango na idadi ya walioelimika (kujua kusoma na kuandika), mkanganyiko wa hali ya muungano wetu na mengineyo.

Haya yote na mengineyo ni mambo ambayo yanahitaji kushughulikiwa sasa na kwa weledi wa hali ya juu, kabla ya kupelekea nyufa zinazojitokeza sasa kugeuka kuwa mpasuko utakaoathiri mustakabali wa taifa letu.

**UTAIFA NA MISINGI:**

Wakati upande mmoja wa Muungano wetu, Tanganyika unakaribia kutimiza miaka 48 tangia kupata uhuru wake, Upande mwengine, Zanzibar kutimiza miaka 46 tangia kufanikisha Mapinduzi na tayari tumeshatimiza Miaka Arobaini na Tano tangia kuasisiwa kwa Tanzania yetu. Kuna ushahidi mkubwa unaotokana na maneno na

matendo ya wengi wetu, kuwa ni ama tumesahau au tumeamua kudharau maana halisi ya UTANZANIA.

Watanzania hivi sasa wamesahau ama wanashindwa kutambua kuwa UTANZANIA ni zaidi ya katiba, sheria ama taratibu na kuwa ni hali kujitambua kuwa sisi ni nani, tunasimamia nini na zaidi ni mfumo kamili wa maisha unaofuata misingi ya uhuru, haki, udugu na amani dhidi ya ubinafsi, uonevu na ubaguzi wa aina yeyote ile uwe wa kipato, kinyadhifa, kikabila, kimaeneo, kidini, kiitikadi, kirangi, kijinsia na kimaumbile.

Hivi sasa hapa kwetu Tanzania;

- Wapo wanaohubiri udini na ukabila ambao wanaojiona ni watanzania.
- Wapo wanaosambaza chuki za kibaguzi ambao wanaojiona watanzania.
- Wapo wanaowanyanyasa wenye kipato kidogo na wasio na madaraka ambao wanaojiona ni watanzania.
- Wapo wanadhulumu roho za kina mama, watoto, wazee na hata walemavu ambao wanaojiona ni watanzania.
- Wapo wanaohubiri siasa za chuki kivyama, kimakundi, kidini, kikabila na kikanda ambao wanajiona kuwa ni watanzania.
- Wapo wanaojihusisha kusuka na kutekeleza mipango mikubwa ya ufisadi dhidi ya hazina ya nchi yetu ambao wanajiona kuwa ni watanzania.

Hawa wote wanajiona ni watanzania. Na zaidi hufikia hata kujiona kuwa wao ni wazalendo zaidi ya wengine.

Katika hali kama hii, ni jukumu letu kukaa pamoja, kukumbushana misingi mikuu ya utaifa wetu kama ambavyo ilivyoasisiwa na kuenziwa na Mwalimu Nyerere, Mzee Karume na waasisi wengine wa taifa letu na pia kujadiliana jinsi tunavyoweza kujirekebisha pale tulipopotea.

**MUUNGANO WETU**

Ndugu wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana

Moja ya mambo muhimu ambayo Mwalimu Nyerere alilisimamia kwa nguvu zake zote ni suala la muungano wetu. Ni wajibu wote sote kama wazalendo wa taifa letu tukawa tayari kujadiliana kwa uwazi na ukweli kuhusu changamoto na hatma ya muungano wetu.

Tunapaswa kutekeleza jukumu hili kwa uadilifu mkubwa kwa minajili ya kuimarisha na kuhakikisha kuwa faida za muungano wetu huu zinawafikia watanzania wote wa pande zote mbili za Muungano. Hili litafanikiwa iwapo tu tutakuwa tayari kuongelea yote yahusuyo muungano wenu kwa kuheshimiana, kuelewana na kukubaliana hata pale ambapo tunatofautiana.

Ni jukumu letu kuhakikisha tunajenga mazingira mazuri na madhubuti ambayo yatahakikisha muungano wetu unadumu na kuimarika kwa faida yetu sote na vizazi vyetu.

**DEMOKRASIA YETU**

Ndugu wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Wote tunakumbuka jinsi gani Mwalimu Nyerere alivyopigania kuanzishwa kwa mfumo wa siasa wa demokrasi ya vyama vingi kinyume cha matakwa ya wengi ndani ya Chama cha Mapinduzi wakati huo. Ni miaka kumi na saba sasa tangia tukubaliane kuanzisha huo hapa nchini mwetu.

Naamini kuwa, wakati tukielekea katika uchaguzi mkuu mwingine hapo mwakani 2010, tunapaswa kukaa pamoja, kujiuliza na kujadiliana kwa undani maswala kadhaa yahusuyo harakati za kuendeleza demokrasia yetu yatakayo tuwezesha kuchanganua na kutambua mafanikio tuliyoyapata na changamoto tunazokumbana nazo hadi sasa na vipi tunaweza kuendeleza ustawi wa mfumo huo.

Baadhi ya masuala ambayo tunayopaswa kujiuliza na kuyajadili kwa umakini mkubwa ni kama vile, baada ya miaka kadhaa ya majaribio, jitihada na mabadiliko kadhaa;

- Je mfumo wetu wa vyama vingi tulionao umewezesha kutupatia uhuru na haki ambazo tulitegemea?
- Je ni kweli dhamira ya kujenga mfumo bora wa demokrasia ya vyama vingi ipo na inatuwezesha kufika pale tunapotegemea kufika?
- Je, tunawezaje kujenga utamaduni wa kidemokrasia miongoni mwetu bila ya kujenga uadui kati yetu?

- Je vipi tunaweza kuuboresha mfumo huu ili utuwezeshe kufikia malengo yetu kama taifa?

Ni pale tu tutakapoweza kuwa na uthubutu wa kujiuliza maswali magumu kama haya na kushirikiana kupata majawabu yake yatakayotuwezesha kuboresha mfumo wetu wa kidemokrasia na ukatuwezesha kutoa msistizo wa ushirikishwaji wa watu katika maamuzi yanayohusu maisha yao kama ambavyo Mwalimu Nyerere alivyoasa.

**JAMII YETU**

Historia ya Taifa letu inaonyesha kuwa, chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere tuliweza kufanikiwa kujenga jamii yenye umoja, upendo na kuaminiana miongoni mwa makundi mbalimbali ya kijamii. Moja ya sifa kubwa juu ya mafaniko ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, ndani na nje ya mipaka yetu, ni lile la kuweza kujenga taifa ambalo watu wake wameweza kuishi pamoja kwa amani na upendo bila ya kujali tofauti zao ziwe za kidini, kikabila, kirangi ama kiasili.

Hata hivyo hali ya mambo inavyokwenda sasa, ni wazi tusipokuwa makini na kuchukua hatua za dhati sasa, sifa hiyo ya umoja na upendo kati yetu itabaki kuwa historia njema iliyopotea.

Ni wajibu wetu sote, hasa viongozi wa kisiasa na kijamii, kuwa makini katika maneno na matendo yetu, ambayo yanaweza kuwa ni sawa kwa mujibu wa maono na maslahi ya

makundi yetu, lakini yakatokea kuwa sumu kubwa kwa umoja na upendo kati yetu na kuhatarisha amani na mstakabali mzima wa taifa letu.

Ni jukumu letu kutumia nafasi hii kuelimishana na kushauriana ni jinsi gani tunaweza kushughulikia changamoto tunazokumbana nazo hivi sasa, kwa njia makini ambazo hazikiuki misingi ya utaifa wetu na kuhatarisha umoja na upendo miongoni mwetu.

**HITIMISHO**

Ndugu wageni waalikwa, mabibi na mabwana

Kwa mara nyingine tena napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwenu nyote kwa kukubali kuja kujumuika nasi katika maadhimisho haya ya kumbukumbu ya maisha ya Baba wa Taifa letu, Mwalimu Julius Nyerere. Pia kwa niaba ya Bodi ya Wadhamini wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere nawashukuru kwa kuja kwenu na kujiunga nasi katika kufanikisha nia ya Taasisi yetu ya Mwalimu Nyerere kuibua na kuchochea mjadala wa kitaifa kuhusu suala zima la UTAIFA wetu na mustakabali mzima wa nchi yetu katika wakati huu ambapo taifa letu linapitia changamoto mbalimbali.

Napenda kuchukua nafasi hii kufungua rasmi mjadala wa mada zetu za leo ambazo zinahusu Watu na Siasa na baadaye mada ya Uongozi, zitakazotolewa na Prof Mwesiga Baregu na Balozi Daudi Mwakawago.

Karibuni